MEZA YA BWANA

Kutangaza Kifo
cha Bwana hadi Kurudi Kwake

YALIYOMO

MEZA YA BWANA –Nyakati za Urejesho ……3

UTIMILIFU WA PASAKA……..…3

UTIMILIFU WA MATOLEO YA KILA SIKU……4

MADHABAHU YA BWANA……6

AGANO JIPYA……..…7

MAAGIZO YA PAULO KUHUSU MEZA YA BWANA……8

KANISA LA KWANZA ULIMEGA MKATE KILA SIKU……...12

HADI KUREJEA KWAKE…….. 13

MASWALI YANAYO ULIZWA KILA MARA…….……14

MEZA YA BWANA

Nyakati za urejesho

Katika **Matendo 3:19-21,** Petero anatuambia kwamba Yesu amepokelewa mbinguni ***"hadi nyakati za urejesho wa vitu vyote"***. Katika siku hizi, Mungu anarejesha **meza ya Bwana** kwenye kanisa. Kwa bahati mbaya meza ya Bwana imepuuzwa kwa makanisa mengi ulimwenguni kote.kwa sababu hiyo kiungo muhimu kwa maisha ya kanisa kimekuwa kikikosekana. Waumini wameibiwa uhalisia wa kukutana na Yesu kwenye meza, ambayo alianzisha. Waumini **wameibiwa kuridhi kwa Baraka(ahadi) za agano jipya.**

Hatujajua sehemu ambayo kula meza hutuweka. Yesu alisema ya kwamba tunafaa kumkumbuka kwa kula mkate na kikombe **(1Kor.11:24-25).** Paulo anasema kwamba ***"ila mara mnapokula huu mkate na kunywa hiki kikombe, mnatangaza kifo cha Bwana hadi kurudi kwake" (*1Kor.11:26).** Hii inamaanisha kwamba kila wakati tunaposhiriki meza ya Bwana, hatukumbuki tu kifo cha Bwana na kupokea ahadi zake na yale tuliopewa kwenye agano jipya, bali pia tunatarajia na kujitayarisha kwa kuja kwake.

UTIMIZO WA PASAKA - Kut.12:1-14

Pasaka ilikuwa sherehe ya kila mwaka iliyosherehekewa na wana wa Israeli kwa ukumbusho wa ukombozi wao kutoka Misri.

Usiku huo BWANA alimwagiza Musa kuwaambia watu kuchukua ***"Mwana- kondoo kwa hesabu ya nyumba"*** **(Kut.12:3);**kumwaga damu ya huyo Mwana-kondoo na kunyunyiza baadhi ya hiyo damu ***"katika miimo miwili na katika kizingiti cha juu,katika zile nyumba watakazomla"*** **(Kut.12:7);** kisha walikuwa ***"wale nyama"*** **(mst.8)** ya Mwana-kondoo**.** Mwana-kondoo ndiye alikuwa sehemu kuu kwenye dhabihu hiyo**.** Ilikuwa awe Mwana-kondoo asiye na mawaa**.**

- **Damu ya mwana kondoo iliwalinda wana wa Israeli kutokana na mharibifu na kuwaletea ukombozi kutoka kwa kifo.**
- **Nyama ya mwana kondoo iliwatia nguvu kwa safari.**
- **Nyumba yote walikombolewa; nymba yote walikuwa wale.**

Usiku ambao Yesu alisalitiwa, alisherehekea pasaka na wanafunzi wake**.** ***"Nao walipokuwa wakila Yesu alitwaa mkate, akabariki, akaumega, akawapa wanafunzi wake akasema, Twaeni, mle; huu ndio mwili wangu. Akakitwaa kikombe, akashukuru, akawapa, akisema, Nyweni nyote katika hiki; kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano jipya, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi"*** **Mat.26:26-28.**

Yesu alifanyika Mwana kondoo wa dhabihu na utimizo wa pasaka wakati damu yake ilimwagika msalabani. ***"Kwa maana Pasaka wetu amekwisha kutolewa kuwa sadaka, yaani, Kristo"*** **(1kor.5:7).** Agizo lake kwa wanafunzi lilikuwa kuchukua mkate, na kuchukua kikombe kwa ukumbusho wake.

UTIMIZO WA SADAKA ZA KILA SIKU

Kut.29:38-46

Chini ya sharia ya Musa dhabihu ya asubuhi na jioni ilikuwa itolewe kila siku. BWANA alimwagiza Musa**, "*Mwana-kondoo mmoja utamchinja asubuhi; na Mwana-kondoo wa pili utamchinja jioni"*** **Kut.29:39.** Pamoja na Mwana-kondoo kulikuwa pia na ***"sadaka ya unga"*** **na** ***"sadaka ya kinywaji"*** **(mst.40).**

Yohana mbatizaji alipomwona Yesu akija, alitangaza **"*Tazama Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu"*** **(Yoh.1:29).** Yesu ndiye ***"Mwana-kondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia"*** **(Ufu.13:8**). Yesu alitimiza sadaka ya kila siku kwa kuwa Mwana-kondoo. Alitupa sadaka ya unga na sadaka ya kinywaji kumkumbuka.

Usiku ambao Yesu alisalitiwa alitua mkate-sadaka ya unga, na akatua kikombe-sadaka ya kinywaji akasema ***"Fanyeni hivi kwa kwa ukumbusho wangu"*** **(Luk.22:19).** Yesu amekuwa Mwana-kondoo wa sadaka, sasa hatufai tena kutoa sadaka ya Mwana-kondoo, lakini ametuachia unga(mkate) na kinywaji.

Bwana ataongea

Sadaka hiyo ilikuwa iteketezwe ***"Mlangoni pa hema ya kukutania mbele ya BWANA"*** na BWANA akasema hapo ndipo **"*nitakapokutana nanyi, ili ninene nawe hapo."* (mst.42).** Tunapokuja kushiriki naye kwa kuleta sadaka ya kila siku, yeye hutimiza neno lake kukutana na sisi na kunena na sisi. Uwepo wake huja na tunaweza kumtarajia kunena na sisi.

- **Chukua wakati kumngojea Bwana katika meza yake**
- **Mtarajie kunena na sisi**
- **Tusiharakishe sherehe ya meza hiyo**
- **Ni mahala pa kukutana na Bwana mwenyewe**

Utakaso

BWANA pia aliahidi kwamba "***Hiyo hema itafanywa takatifu na utukufu wangu"* (mst.43).** Katika Agano jipya tunakuja kuelewa kwamba sasa sisi ndio hema/hekalu/makao ya Mungu. "***Hamjui ya kuwa nyinyi mmekuwa hekalu la Mungu; na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu?"* 1Kor.3:16.** Tunapokutana na Bwana katika meza yake, tunajua kwamba tumetakaswa kwa damu yake. Atakutana na watu wake;Utukufu wake utakuwepo.

Mungu atakaa na watu wake

Kisha Mungu anaahidi**, "*Nami nitakaa kati ya wana wa Israeli, name nitakuwa Mungu wao. Nao watanijua kuwa mimi ndimi BWANA, Mungu wao"* (Kut.29:45-46).** Ahadi hizi ni vipengele vya Agano jipya vilivyorejelewa katika **Yeremia 31:34.**

Ni kwa msingi gani ambapo Mungu atakaa kwa kanisa lake na kusema sisi ni watu wake? Ni kwa sababu tunashiriki katika sadaka ya kila siku ya mwili na damu ya Yesu kama Mwana-kondoo aliyechinjwa ambaye hutuletea wokovu. Hii huonyesha ya kwamba tumetoka katika ulimwengu na tunajitenga kwa Mungu.Tunatakaswa na utukufu wake tunapokutana na yeye kila siku na kushirikiana na yeye. Tunafaa kuja kwake asubuhi na jioni kutambua yale ambayo amefanya na kutoa shukurani kwa wokovu wetu.

MADHABAHU YA BWANA

Meza yaBwana ni Zaidi sana ya sherehe au mlo wa ukumbusho. Ni wakati wa kurejesha madhabahu ya Bwana.Hii ndiyo njia ya ushindi na uhuru kutoka kwa ufungo wa kipepo unaoletwa na watu kuhudhuria meza ya mapepo na kula kutoka kwa sadaka inayotolewa kwa mapepo **(1Kor.10:20-21).** Wale ambao huenda kwa meza ya mapepo mara kwa mara kupitia kwa waganga au makuhani wa mapepo, hula sadaka iliyotolewa kwa huyo pepo, na kwa hiyo huweka mapepo ndani yao, na kupagawa kutoka wakati huo.

Ni mara ngapi Zaidi tunafaa kushiriki mwili na damu ya Bwana Yesu Kristo,kushikilia sadaka yake na maisha ya ufufuo wake.Hii inatuwezesha kwa kweli kuishi na kuenenda katika ushirika wa mwili na damu yake pamoja na ndugu katika mwili wa Kristo.Hii hufuta na kuvunja agano lolote la kipepo na kubadilisha ya kipepo na kile kilicho kweli,takatifu na kiungu.

Kikombe na mkate: Ushirika ndani ya Kristo

Paulo anafundisha kwamba "***Kikombe kile cha Baraka tukibarikicho…ni ushirika wa damu ya Kristo! Mkate ule tuumegao…ni ushirika wa mwili wa Kristo!*** **(1Kor.10:16).** Kwa kweli, meza ya Bwana ni ushirika [neno ushirika ni koinonia] wa mwili na damu wa Yesu Kristo. Kwa kushiriki kwa meza ya Bwana, tunatambua kwamba "***sisi tulio wengi tu mwili mmoja; kwa maana sisi sote twapokea sehemu ya ule mkate mmoja"*** **(mst.17).**

Ulaji wa dhabihu

Tunaposhiriki katika meza ya Bwana, tunakula sadaka ya mwili na damu yake na kwa hiyo tunakuwa "***washirika wa madhabahu"*** **(mst.18).** Ni wakati wa kutambua kwamba meza ya Bwana ndiyo madhabahu muhimu ambayo Bwana ametupatia katika Agano jipya. Inachukua mahala pa madhabahu ya Agano la kale na ndani ya kusherehekea meza ya Bwana, kuna utimizo wa kina wa kiagano ndani wa yote ambayo Mungu aliahidi katika Agano la kale.

Urejesho wa meza ya Bwana

Urejesho wa meza ya Bwana ndiyo suluhisho kwa upotovu na ugandamizi wa uganga ambao hufunga watu wengi na hata serikali katika nchi za Afrika, na nchi zingine. Kuna madhabahu mengi ya kipepo na maagano ya kipepo ambayo yamefanywa na ambayo huendelea kufunga watu na hata mataifa.Meza ya Bwana imepuuzwa karibu ulimwenguni kote ***na*** makanisa na viongozi hawajaelewa umuhimu kuu wa meza ya Bwana.Yesu alisema, "***Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu;fanyeni hivi kila mnywapo ,kwa ukumbusho wangu"*** **(1Kor.11:25).**

Katika madhabahu Yesu ameinuliwa

Katika **Yohana 3:14** Yesu alisema, ***"Na kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa"***. Hii inarejelea **Hesabu 21:6-9**, ambapo wana wa Israeli walikuwa wameongea dhidi ya Mungu, na BWANA akatuma ***"nyoka za moto kati ya watu, wakawauma, watu wengi wakafa*****(mst.6).** BWANA akamwagiza Musa "***Jifanyie nyoka ya shaba, ukaiweke juu ya mti, na itakuwa kila mtu aliumwa, aitazamapo ataishi"*** **(mst.8).**

Tena katika **Yohana 12:32** Yesu alisema "***Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu." "Aliyanena hayo akionyesha ni mauti gani atakayokufa"*** **(mst.33).** Katika meza ya Bwana tunakumbuka kifo cha Yesu kwenye msalaba. Tunapomwangalia na kukubali yale ambayo ametufanyia kupitia kwa kumwaga damu yake, tunapokea wokovu, uponyaji na ukombozi.

AGANO JIPYA

Katika maelezo ya meza ya Bwana ilivyonakiliwa kwetu sisi katika **Mathayo, Mariko** na **Luka,** na katika maelezo ya Paulo katika **1Kor.11,** Yesu anazungumza juu ya damu yake kuwa damu ya ***"agano jipya".*** Hii agano jipya ilitabiriwa na Yeremia katika **Yeremia 31:31-34,** na limerudiwa katika **Waebrania 8:8-12.**

Yesu alikuwa akirasimisha agano jipya. Agano la kale na mfumo wake utoaji sadaka ya umwagikaji wa damu ya fahali na mbuzi; na wakuhani mkuu kupeleka damu kwenye Mahali patakatifu Zaidi mara

moja kwa kila mwaka, kulipia dhambi za watu, imetupiliwa mbali. ***"Kwa kule kusema, Agano jipya, amelifanya lile la kwanza kuwa kuukuu"*** **(Ebr.13:8).**

Kuna ahadi nne za ajabu za agano jipya ambazo tunaweza kupokea na kuenenda ndani yake, kila mara tunaposhiriki meza ya Bwana. Ni muhimu kwa kanisa kuelewa kwamba uhusiano wetu na Mungu ni wa kiagano. Mungu ndiye hufanya agano na sisi na limetiwa muhuri kwa damu ya Yesu. Kwa hiyo agano hilo halivunjiki, kwa sababu Yesu alimwaga damu yake. Tunaweza kutegemea ahadi ambazo ameweka.

Kila mwuumini anafaa kujua kwamba kuna ahadi nne zilizo wazi ambazo ziko katika kiini cha agano jipya kufunua mapenzi ya Mungu kwetu na kujulisha upendo wake mkuu kwetu.

Ahadi za agano jipya - Ebr.8:10-12

1. **"*Nitayaweka sheria zangu kwenye nia zao na kuziandika kwenye mioyo zao***
2. ***Nitakuwa Mungu wao nao watakuwa watu wangu***
3. ***Wote watanijua mimi, kutoka kwa mdogo wao hadi mkubwa wao***
4. ***Nitawasamehe maovu yao na dhambi zao sitazikumbuka tena"***

MAAGIZO YA PAULO KWA MEZA YA BWANA

Ruwaza timilifu

Katika **1Korintho 11,** Paulo alileta marudio mazito kwa kanisa kuhusu uzoefu wao kwa meza ya Bwana (**mst.17-22).** Alisema kwamba uzoefu wao haukuwa meza ya Bwana (**20).** Kisha katika **mistari 23-25,** Paulo anatuletea kile alipokea kutoka kwa Bwana. Paulo yuko wazi kabisa: anatufundisha sawasawa kile amepokea kutoka kwa Bwana. Maneno yake yanafanana na yale yaliyonakiliwa katika Injili za Mathayo, Mariko na Luka, lakini Roho Mtakatifu alikuwa amempa Paulo ufahamu kamili wa meza ya Bwana na yale ambayo Yesu alikuwa amukusudia.

Mara kwa mara?

Kulingana na Paulo, Yesu alisema, ***"Fanyeni hivi kila mara mnapokunywa, kwa ukumbusho wangu"*** **(1Kor.11:25).** Tunafaa kumkumbuka Yesu, **mara kwa mara tunapokunywa kikombe.** Kisha

Paulo anasema "***Maana kila mulapo mkate huu na kunywea kikombe hiki"*** **(mst.26).** Mara kwa mara ni kiasi gani? Ni mara ngapi tunafaa kumkumbuka Yesu na yale ambayo alifanya kupitia kwa sadaka ya kifo chake msalabani? Hakuna mpaka kwa mara ambazo tunaweza kushiriki mkate na kikombe. Inafaa kuwa sehemu muhimu ya ushirika wetu pamoja.

Damu ya Yesu ya ukombozi

Meza ya Bwana inatufanya kulenga yale Yesu alifanya kwa kufa msalabani, kulenga yale aliyoyatimiza. Andiko linasema, ***"Lakini Kristo akiisha kuja, aliye kuhani mkuu wa mambo mema yatakayokuwapo … wala si kwa damu ya mbuzi na ndama, bali kwa damu yake mwenyewe aliingia mara moja tu katika patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele"*** **Ebr.9:11-12.** Baada ya kufufuka kutoka kwa wafu Yesu alipeleka damu yake kwa hema ya kimbinguni.

Si kwa njia isiyostahili

Paulo anatuonya kwamba hatufai kula mkate huo au kunywea kikombe hicho cha Bwana "***isivyostahili"***; tukifanya hivyo "***tutakuwa tumejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana"*** **(1Kor.11:27)**. *'Isivyostahili'* inamaanisha *kutoheshimu;* inamaanisha *kutofahamu umuhimu unaoashiriwa na meza hii.* Yesu alisema tunafaa kumlenga yeye.Hatufai kulenga kutostahili kwetu,bali kulenga na kufurahia yale Yesu ametufanyia kwa kwenda msalabani.

Mtu ajihoji mwenyewe

Paulo alisema ***"Mtu ajihoji mwenyewe"*** **(mst.28).** Neno 'kujihoji' linamaanisha *kujaribu, kuidhinisha;* lina *maana ya kukubalika.* Ni kwa msingi gani tunakubalika? Ni kwa msingi gani tunaweza kuendelea mbele kula na kunywa? Paulo alisema mara mtu akiisha kujihoji, ***"na hivyo aule na kukinywea kikombe"*** **(mst.28).**

Tunakubalika kwa kumwamini Yesu Masiha, na yale Yesu ametufanyia. Damu yake hutusafisha kutokana na dhambi zote. Tunaweza kujua kupitia kwa imani kwa neno la Mungu kwamba tunakubalika na kwa hivyo tunaweza kula mkate na kunywea kikombe inavyostahili.

Paulo anatupa jaribio jepesi katika **2Korintho 13:5, "*Jijaribuni wenyewe kwamba mmekuwa katika Imani; jithibitisheni wenyewe. Au hamjijui wenyewe, kwamba Yesu Kristo yu ndani yenu?"***

Hili ndilo jaribio: je, unaamini? Umezaliwa mara ya pili? Je, Yesu Kristo anaishi kwa roho yako kwa imani? Kama ni hivyo, unakaribishwa kwa meza kula na kunywa mwili na damu ya Bwana.

Hukumu

"*Maana alaye na kunywa, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua ule mwili"* (1Kor.11:29). Hukumu hiyo inakuja yenyewe. Usipokula na kunywa kwa imani basi hauli na kunywa kwa njia inayostahili. Hukumu hiyo ni nini? ***"Wengi kwenu walio hawawezi na dhaifu, na watu kadha wa kadha wamelala*** [kifo cha mapema]***"* (mst.30).**

'Kupambanua'mwili wa Bwana ni nini?

Ni nini huleta hii hukumu? Jibu ni "***kutokuupambanua mwili wa Bwana"* (mst.29).** Hili '*kupambanua'* linatafsiriwa mahali pengine kwenye Andiko kama *'kuwa na tashwishii au shaka'.*

Mifano ya hili neno la kigiriki linalitafsiriwa kama 'kuwa na tashwishi':

1) ***"Roho akaniambia nifuatane nao, nisione tashwishi"* Matendo 11:12.** Petero alikuwa anaongozwa na Roho kwenda kwenye eneo asilolijua; alikuwa aende na kumhubiri Yesu kwa nyumba ya watu wa Mataifa.Lazima angalienda, akiamini kabisa yale maono ambayo Mungu alimwonyesha, bila kuwa na tashwishi. Kama angekuwa na tashwishi, hangefaulu.
2) "***Ila aombe kwa imani, pasipo shaka yoyote; maana mwenye shaka ni kama wimbi la bahari lililochukuliwa na upepo"* Yak.1:6.** Mtu amwombaye Mungu akiwa na shaka moyoni hatajibiwa maombi yake. Tunafaa kuomba kwa imani.
3) Kupitia kwa kuulani mtini, Yesu alikuwa akifundisha kwa mamlaka makuu juu ya imani. Alisema, ***"Amini nawaambia, mkiwa na imani, msipokuwa na shaka, mtafanya si hilo la mtini tu, lakini hata mkiuambia mlima huu, Ng'oka, ukatupwe***

baharini, litatendeka" **Mt.21:21.** Yesu alisema, ***"Na yoyote mtakayoyaomba katika sala mkiamini, mtapokea.*** **mst.22.**

Bila shaka

Kwa sababu hatupambanui mwili wa Bwana, hukumu huja kwetu ***"Kwa sababu hiyo wako wengi kwenu walio hawawezi na dhaifu, na watu kadha wa kadha wamelala"*** **(1Kor.11:30).** Kutokupambanua mwili wa Bwana [kutokana na kigiriki] inaweza kusomwa kama **kuwa na shaka.** Shida ambayo kanisa iko nayo ni kwamba kwa jumla sisi hupuuza kusherehekea meza ya Bwana, na hata kuishiriki kwa kutofuata kanuni ya mara kwa mara, hatujaupambanua mwili wa Bwana; kwa maneno mengine tumetia shaka ukombozi kamilifu ambao Mungu anatupa ndani ya Kristo na kupitia kwa Kristo.

Kwa kutupatia mkate huo na kikombe hicho kwa kumkumbuka nayo, Yesu anatupatia ufunguo wa ajabu wa kupokea na kuishi ndani ya ufalme, kwa kufahamu vyema ukamilifu wa yale alifanya kwa kuwa Mwana-kondoo wa sadaka na kutoa maisha yake msalabani.

Kula na kunywa kwa Imani

Kila wakati tunapokuja kwa meza ya Bwana tunafaa kuja kwa imani, bila kuwa na shaka kwa mwili wa Bwana; si kupunguza umuhimu wa kiini cha yale Yesu amefanya kupitia kwa msalaba.Tunapotubu na kuja kwa utiifu kumkumbuka Yesu, ***"kila mara mnapokunywa"***, tutaingia upeo wa juu wa imani na ukweli wa Kristo kukaa ndani ya mioyo yetu na kuachilia neema yake na uweza wake ndani ya maisha yetu,kufanya mapenzi yake,na kujitayarisha kwa kuja kwake.

- Tunapaswa **kuamini kwa moyo wote,** bila shaka, kwa kazi kamilifu ya Yesu kupitia kwa msalaba.
- Tunapaswa kuamini kikamilifu ya kwamba Yesu alienda msalabani kama Mwana –kondoo wetu wa Pasaka.
- **Dhambi zetu zimeondolewa kikamilifu** na hatuna haja tena kutembea kwa aibu, kama walio na hatia na lawama.
- Kuamini na kupokea yale Yesu alitufanyia msalabani **hutuleta kwa uzima wa milele.**

- Lakini **kama tuna shaka**, kutoamini, kutopambanua mwili na damu ya Bwana, **tunapitia mauti.**
- Tumefanywa **wa kukubalika kwa Mungu,** kupitia kwa imani katika mwili na damu ya Yesu.
- Tunapaswa **kula na kunywa kwa heshima kuu,** kutambua kikamilifu umuhimu wa mlo huu wa ukumbusho.
- Basi na tuje kwa imani, **bila kushuku ukweli** wa yale Yesu alifanya kwa kukubali mwili wake uvunjwe kwa ajili yetu.

KANISA LA KWANZA WALIMEGA MKATE KILA SIKU

Katika **Matendo 2:42** tunapata ***"Kuumega mkate"*** ilikuwa mojawapo ***"kazi za kwanza"*** ambayo kanisa la kwanza ***"lilidumu imara"*** kwayo. Huu ulikuwa uzoefu wa kila siku na ulifanyika kwa nyumba. ***"Na siku zote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu, wakimega mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe"*** **mst.46.**

Wakristo wa kwanza walikutana kila siku kwa nyumba na kumega mkate kila siku kwa nyumba. Hata ingawa kuna ushahidi ya kwamba makanisa baadaye walichukua siku ya kwanza ya wiki [Jumapili] kama wakati spesheli kukutana kuumega mkate (**Matendo 20:7),** ni dhahiri kwamba kanisa la kwanza walimega mkate kila siku nyumbani.

Muhimu kwa urejesho wa ukristo wa kitume ni urejesho wa **kumega mkate nyumbani kati ya waumini wakati wowote wanapokutana.**

Cha umuhimu Zaidi

Kushiriki meza ya Bwana inapaswa kuwa kitu cha umuhimu zaidi kwa maisha ya kanisa.Kusherehekea meza ya Bwana ni umuhimu wa msingi,kwa kuwa ni mojawapo ya kazi za kwanza za kanisa.Kanisa la kwanza "***walidumu katika fundisho la mitume,na katika ushirika,na katika kuumega mkate,na katika kusali."*** **Matendo 2:42.**

Bwana anarejesha kwa kanisa lake ushirika wa mwili na damu ya Yesu.Kimaandiko hakuna kipimo cha **kiasi cha mara ngapi** tunashiriki meza ya Bwana au komunyo. Ni wakati ambapo tunamlenga Yesu, tukikumkumbuka tunapokuwa na ushiriki nayeye. Kumega mkate

kunaweza kufanyika nyumbani au mahali popote ambapo wawili au watatu au wengi wanapokutana katika jina lake (**Mt.18:20).** Makanisa mengine wameongeza sheria nyingi kwa kumega mkate; ni wakati wa kurudi kwa uzoefu wa kimaandiko. Hii ni muhimu kwa ufufio na urejesho.

Ukumbusho wa nini?

Tunapaswa kufanya kitu! Tunapaswa kufanya nini? Tunapaswa kula mkate na kunywa kutoka kwa kikombe na kumkumbuka Yesu, yaani, kumkumbuka Yesu kwa yale alitufanyia kwa kwenda msalabani: ***"Alijitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya wote"*** **(1Tim.2:6); Waebrania** inasema, ***"akiisha kufanya utakaso wa dhambi,aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu"*** **(Ebr.1:3).** Tunapaswa kumkumbuka Yesu kwa yale alifanya kwa kufa msalabani na kufufuka kutoka kwa wafu. Paulo anasema kwamba tunapomkumbuka Yesu kwa mkate na kikombe, tunatangaza kifo chake, lakini si kifo chake tu; tunatangaza ufufuo wake na kupaa na kurudi kwake.

HADI KURUDI KWAKE

Meza ya Bwana inahusu kurudi kwake

Tunapokula mkate na kunywa kikombe, Andiko linasema, ***"mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo"*** **(1Kor.11:26).** Hiki ndicho kipindi katika historia ambacho tunaishi, yaani, kipindi tangu Bwana alipokufa msalabani hadi arudi.

Kwa kunikumbuka

Meza ya Bwana ni zaidi kukumbuka kifo cha Bwana! Ni kumkumbuka Bwana mwenyewe, ambaye alikufa na kufufuka tena, na ambaye ***"atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu"*** **(1The.4:16).** Kutakuwa na kizazi ***"tulio hai, tutakaosalia hata wakati wa kuja kwake Bwana"*** **(mst.15).** Bwana Yesu atakaporudi ***"Mungu atawaleta pamoja naye wale waliolala katika Yesu"*** **(mst.14).**

Kujitayarisha kwa kuja kwake

Utamatisho wa historia sio sisi wote kuifikia mbinguni, bali ni kwa kujitayarisha kwa kurudi kwa Bwana, ambaye anarudi katika nchi.

Kuja kwa Bwana inapaswa kuwa kiini na jambo muhimu katika imani yetu. Tunaokolewa kwa imani [kuamini] katika kazi ya ukombozi ambayo Yesu alimaliza kwa kufa na kufufuka tena, lakini tumeokolewa kwa sababu gani? Kimsingi, hatujaokolewa kwenda mbinguni; tumeokolewa kuwa ndani ya Kristo na kushuhudia Kristo na kuangaza maisha ya Kristo hapa duniani, hadi arudi.

Hatujitayarishi kwenda mbinguni, bali tunajitayarisha kwa kurudi kwa Bwana.Huu ndio ukweli tunaokumbushwa kila wakati tunaposhiriki meza ya Bwana.

Kila wakati tunaposhiriki meza ya Bwana
Tunatangaza kwamba Yesu alikufa, kwamba alifufuka kutoka kwa wafu, Na kwamba anarudi tena, Hallelujah!

MASWALI AMBAYO YANAULIZWA MARA KWA MARA

Na watoto je?

Je, watoto wanakaribishwa kula na kunywa katika meza ya Bwana? Hakuna maagizo ya moja kwa moja katika Maandiko.Tunajua kwamba Yesu aliwakemea wanafunzi kwa kuwakataza watoto kuja kwake. ***“Lakini Yesu akasema, waacheni wadogo waje kwangu; wala msiwazuie; kwa maana walio mfano wa hao, ufalme wa Mungu ni wao. Akaweka mikono yake juu yao”*** **(Mt.19:13-15).**

Tunapaswa kujiuliza: je, mtoto anaweza kuwa na imani kuokolewa? Kama ndiyo, nini inawazuia kula na kunywa.

Wana wa Israeli walipoadhimisha Pasaka ya kwanza kule Misri, familia yote ilihusika. Wote walilindwa kwa damu ya Mwana-kondoo, na wote walikuwa wale nyama ya Mwana-kondoo (**Kut.12).** Je, unaweza kufikiria juu ya wazee na kina baba wakiwakataza watoto kula nyama ya Mwana-kondoo?

Je, lazima mtu abatizwe ndipo aweze kushiriki meza ya Bwana?

Tena Maandiko yamekimya, lakini tarajio la kawaida la Andiko ni kwamba mtu anapomwamini Yesu Kristo, anabatizwa mara na kisha kuendelea katika kumega mkate, kila siku na kutoka kwa nyumba hadi nyumba **(Matendo 2:41-46).** Makanisa mengi ya kisasa na huduma hawabatizi waumini wapya mara na kwa hivyo wanakabiliana na swali la 'je, mtu asiyebatizwa anafaa kushiriki'?

Tena tukiangalia ruwaza ya hadithi ya Kutoka, wale waliokula nyama ya Mwana-kondoo na kulindwa na damu, hawakubatizwa kabla kula. Bibilia inasema walibatizwa ndani ya Musa kwa kupitia kwa Bahari ya shamu **(1Kor.10:2).**

Ni vitu gani vinaweza kutumika?

Yesu alichukua mkate, na akachukua kikombe. Haisemi hasa katika Agano jipya ya kwamba kulikuwa na divai kwenye kikombe. Yesu alirejelea ***"tunda la mzabibu"*** **(Lk.22:18, Mk.14:25, Mt.26:29).**

Makanisa ya madhehebu ya zamani kwa jumla hutumia divai ya pombe, wakiamini kwamba hiyo ndiyo uzoefu katika Maandiko. Mengi ya madhehebu mapya hutumia maji ya matunda ya mzabibu. Maandiko hayabainishi asili ya yale yaliyo ndani ya kikombe,kama ilikuwa na pombe au haikuwa na pombe.Kwa hivyo hatupaswi kuwa na mabishano kuhusu ya kinywaji kitakachotumika.

Makanisa mengi waliozaliwa mara ya pili na kujazwa Roho hutumia maji ya matunda ya mzabibu au kinywaji kilicho na rangi. Na soda au vinywaji vingine vya rangi je? Na chai je?

Watu waonaishi kwenye vijiji vilivyotengana mbali na miji, watanunuaje mkate na maji ya matunda ya mzabibu kama hakuna duka na mkate si sehemu ya chakula chao cha kawaida, wala hawapandi mizabibu?

Lazima tuyajibu haya maswali kwa utendaji na kutambua kuwa meza ya Bwana ni wakati wa kumkumbuka, tunapokula na kunywa kwa njia ya kumlenga yeye.

Kama Yesu angekuja kwa nyumba yako kijijini na kile mbacho ungemwandalia ni chakula ambacho wewe hula kwa kawaida na kinywaji

chako cha kawaida, hata kama ni maji, je Yesu angekula na kunywa na wewe? Na je, angekataa kula na kunywa na watoto wako?

Fikiria juu ya mambo haya, na usitegemee sheria za kidini ambazo umeziridhi kutoka kwa Wamisionari waliotangulia hapo mbele.

Fundisho hili la meza ya Bwana linaitisha urejesho wa meza ya Bwana, kwa kuwa hii ndiyo madhabahu katika Agano Jipya. Ni madhabahu ya dhabihu. Kupitia kwa kula na kunywa mwili na damu ya Yesu, tunashiriki katika dhabihu.

Yesu alisema kwamba kikombe kilikuwa damu ya Agano Jipya.Tunapaswa kufanya upya ufahamu wetu wa asili ya kiagano ya meza ya Bwana, na kupokea upya ahadi za Agano Jipya.

Fundisho hili linahutubia kutoelewa kwa ‘kujihoji mwenyewe’na linatufundisha jinsi ya kula na kunywa inavyostahili, ili kupokea Baraka ya afya na nguvu na uzima, na ili tusije chini ya hukumu.

Hiki kijitabu kimeandikwa na Janet na Paul Galligan,

Revival ministries, Australia.

Revival Ministries, Australia huhudumia mataifa

Kupitia SHILOH International Apostolic Ministries.

Kimetafsiriwa na Dorothy Akinyi Otieno.